# YANIPASA KUMSHUKURU MUNGU

*M.Makonge*




1.Nitamsifu kwa kila machungu,
Maa-na yeye kanifanyanilivyo,
Nitamsifu kwa upofu wangu,
Maa-na yeye kanifanynilivyo.

2.Nitamsifu kwa ukoma wangu, Ee- Ee,
Maa-na yeye kaniumba nilivyo, Ee- Ee,
Ingawa watu wananite-nga, Ee- Ee,
Sitaachakumsifu muumba, Wa-ngu.

3.Nitamsifu kwa ugumba wangu, Ee- Ee,
Maa-na yeye kaniumba nilivyo, Ee- Ee,
Ingawa watu wanicheka sana, Ee- Ee,
Sitachoka kumsifu Muumba, Wa-ngu.

4.Nitamsifu kwa magonjwa yangu, Ee- Ee,
Maa-na yeye anajua yote, Ee- Ee,
Ingawa watu wananitenga, Ee- Ee,
Yeye atanipokea kwake, Mbinguni.